



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI  
MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI



**TAARIFA KWA UMMA**  
**WIKI YA USALAMA WA RELI TANZANIA**  
**TAREHE 10-16 OKTOBA, 2022**

Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA) inautangazia umma kuwa Wiki ya Usalama wa Reli Tanzania itaadhimishwa Nchini kuanzia tarehe 10-16 Oktoba, 2022. Maadhimisho hayo yatazinduliwa rasmi na Mhe. Prof. Makame Mnyaa Mbarawa (Mb), Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi.

Tunapoadhimisha Wiki hii, tunawahimiza watumiaji wa huduma za reli na wananchi wote kwa jumla wawe makini, waangalifu na wachukue hadhari za kiusalama wakati wote wanapotumia huduma za reli wakiwa kwenye vituo vya reli, ndani ya mabehewa na hata wanapopita kwenye maeneo ya reli. Ni muhimu kufahamu kwamba treni zinakwenda kwa mwendo kasi na zinaweza kukawia au kushindwa kusimama ghafla inapotokea dharura. Hivyo basi, ni wajibu wa kila mwananchi kuchukua tahadhari ili kuokoa maisha.

LATRA ikiwa ni Mdhibiti wa Huduma za Usafiri wa Reli Tanzania, kwa kushirikiana na Shirika la Reli Tanzania (TRC) pamoja na Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA), ina wajibu wa kuhakikisha kuwa huduma za usafiri wa reli hapa Nchini zinatolewa kwa ubora na usalama kwa watuamiaji na wananchi kwa jumla.

Kwa wananchi wanaoishi maeneo inakopita reli na Watanzania wote kwa jumla, LATRA inasisitiza watumie wiki hii kukumbushana umuhimu wa kutunza na kulinda miundombinu ya reli pamoja na mazingira kwa maendeleo ya Nchi yetu. Tuunge mkono juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika uwekezaji mkubwa unaoendelea ili kuboresha miundombinu ya reli na kukuza uchumi wa Tanzania.

Maadhimisho ya Wiki ya Usalama wa Reli yanaongozwa na Kaulimbiu: **“Chukua Tahadhari, Treni Zina Mwendo Wa Haraka, Ni Hatari”**

Imetolewa na;  
**CPA Habibu J. S. Suluo**  
**Mkurugenzi Mkuu**  
**7 Oktoba, 2022**